***SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR***

**TUME YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA**

# RIPOTI YA TATU YA UTEKELEZAJI WA KAZI ZA TUME YA MAADILI KWA MWAKA 2018/2019

copy

**Septemba, 2019**

(Imewasilishwa kwa mujibu wa Kifungu cha 29 cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Nam. 4 ya 2015)

JADWELI, MICHORO NA VIAMBATANISHO ........ 4
1.0 UTANGULIZI ........ 9
1.1 DIRA ........ 9
1.2 DHAMIRA ........ 9
1.3 MAADILI YA MSINGI ........ 10
1.4 LENGO KUU ........ 10
2.0 MUUNDO WA TUME YA MAADILI ........ 11
2.1 IDARA ZA TUME YA MAADILI ........ 12
2.2 WATUMISHI WA TUME YA MAADILI ........ 12
2.3 MAJUKUMU YA TUME YA MAADILI ........ 14
2.4 MAMLAKA NA UWEZO WA TUME YA MAADILI ........ 16
3.0 KAZI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KWA MWAKA 2018/19 ........ 17
4.0 UTEKELEZAJI HALISI WA KAZI ZA TUME YA MAADILI KWA MWAKA 2018/2019 ........ 17
4.1 TAMKO LA MALI NA MADENI YA VIONGOZI WA UMMA ........ 17
4.1.1 Uchapishaji na Usambazaji wa Fomu ya Tamko la Mali na Madeni ........ 18
4.1.2 Uchambuzi wa Fomu ........ 18
4.1.3 Kutangaza Majina ya Viongozi wa Umma katika Gazeti Rasmi la Serikali ........ 20
4.1.4 Ufuatiliaji na Ukusanyaji wa Taarifa za Viongozi Wasiojaza Fomu ........ 21
4.2 MFUMO WA KIELEKTRONIKI WA KUSAJILI TAARIFA ZA MALI NA MADENI YA VIONGOZI WA UMMA ........ 21
4.3 UHAKIKI WA TAARIFA ZA MALI NA MADENI YA VIONGOZI WA UMMA ........ 22
4.3.1 Uchambuzi wa Taarifa za Uhakiki ........ 22
4.3.2 Mgongano wa Kimaslahi ........ 25
5.0 KUPOKEA NA KUFANYA UCHUNGUZI WA TUHUMA NA MALALAMIKO YA UKIUKWAJI WA SHERIA YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA ........ 25
5.1 Uchambuzi wa Malalamiko ........ 26
6.0 KUJENGA UELEWA KWA WANANCHI NA VIONGOZI WA UMMA UNGUJA NA PEMBA KUHUSU MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA ........ 27
6.1 Mikutano na Viongozi wa Umma ........ 28
6.2. Mikutano na Wananchi na Wanafunzi ........ 28
6.3 Utayarishaji na Urushaji wa Vipindi vya Elimu na Matangazo kupitia Vyombo vya Habari ........ 29
6.4 Utoaji wa Vipeperushi, Machapisho na Matangazo ........ 30
7.0 MAADHIMISHO YA SIKU YA MAADILI ........ 30

copy

8.0 KUWAPATIA MAFUNZO YA KITAALAM WATUMISHI WA TUME YA MAADILI ....32
9.0 KUTAYARISHA MPANGO MKAKATI WA TUME YA MAADILI KWA KIPINDI CHA MIAKA MITANO ....33
10.0 VIKAO VYA TUME ....33
11.0 HALI YA UPATIKANAJI WA FEDHA ....34
12.0 VIKWAZO NA UTATUZI WAKE ....35
13.0 MIKAKATI YA TUME YA MAADILI KWA MWAKA 2019/2020 ....37
14.0 MAPENDEKEZO ....38
15.0 HITIMISHO ....39
16.0 UWASILISHAJI WA RIPOTI ....40

copy

## JADWELI, MICHORO NA VIAMBATANISHO

### JADWELI

Jadweli Nambari 1: Idadi ya Watumishi wa Tume ya Maadili na Viwango vyao vya Elimu........................................................................................ 14

Jadweli Nambari 2: Muhtasari wa Uwasilishaji wa Fomu ........................... 19

Jadweli Nambari 3: Uhakiki kwa Viongozi wa Umma kwa mwaka 2018/2019 ........................................................................................ 23

Jadweli Nambari 4: Idadi ya Malalamiko iliyopokelewa 2018/2019 ............. 26

Jadweli Nambari 5: Mikutano ya Viongozi, Wananchi na Mabaraza ya Vijana waliopatiwa Elimu ya Kukuza Maadili ................................................ 29

Jadweli Nambari 6: Idadi ya Watumishi Waliopatiwa Mafunzo .................... 33

Jadweli Nambari 7: Hali ya Upatikanaji wa Fedha..................................... 35

### MICHORO

Mchoro Nambari 1: Muhtasari wa Uwasilishaji wa Fomu ........................... 20

Mchoro Nambari 2: Uhakiki kwa Viongozi wa Umma kwa mwaka 2018/2019 ........................................................................................ 24

Mchoro Nambari 3: Hali ya Upatikanaji wa Fedha..................................... 35

### VIAMBATANISHO

Kiambatanisho Nambari 1: Muundo wa Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma........................................................................................ 41

Kiambatanisho Nambari 2: ORODHA YA VIONGOZI WA UMMA ................. 42

Kiambatanisho Nambari 3: 1 Malalamiko yaliyopokelewa Julai-Juni 2018/2019 ........................................................................ 44

copy

## MAELEZO YA MWENYEKITI

Hii ni Ripoti ya Tatu ya Utekelezaji wa kazi za Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Ripoti hii imetayarishwa kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 29 cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Nam. 4 ya 2015, kinachoeleza kwamba:

> "29(1) Mwenyekiti atatayarisha Ripoti ya Mwaka na kuiwasilisha kwa Rais ndani ya kipindi cha miezi mitatu baada ya mwisho wa mwaka wa fedha husika.
>
> (2) Ripoti ya Mwaka itajumuisha maelezo kuhusu utekelezaji wa kazi za Tume.
>
> (3) Baada ya kupokea Ripoti chini ya kifungu cha (1) cha kifungu hiki, Rais atamtaka Waziri kuiwasilisha Ripoti hiyo mbele ya Baraza la Wawakilishi katika kikao kijacho".

copy

Tume ya Maadili imepewa jukumu la kusimamia Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Nam. 4 ya 2015. Miongoni mwa majukumu ya Tume ya Maadili ni kupokea, kusajili na kufanya uhakiki wa Tamko la Mali na Madeni kutoka kwa Viongozi wa Umma. Aidha, Tume ya Maadili hupokea na kufanya uchunguzi wa malalamiko au tuhuma za ukiukwaji wa maadili dhidi ya Viongozi wa Umma na kutoa elimu kwa umma na Viongozi kuhusu umuhimu wa kuimarisha Maadili. Hivyo, ninapenda kuchukuwa fursa hii kuelezea kwa ufupi utekelezaji wa majukumu hayo, mafanikio na changamoto zilizojitokeza.

Katika kipindi hiki cha utekelezaji, Tume ya Maadili imepokea na

kusajili Fomu za Tamko la Mali na Madeni 1,702 ikilinganishwa na Matamko 1,664 katika mwaka uliopita 2017/18 na 1,620 katika mwaka wa 2016/17 wakati ilipoanzishwa. Aidha, katika kipindi hiki cha utekelezaji idadi ya viongozi waliochelewa kuwasilisha Fomu za Tamko ni 26 ikilinganishwa na 25 katika mwaka 2017/18 na 141 katika mwaka wa kwanza wa kuanzishwa kwa Tume ya Maadili 2016/17. Takwimu zinaonesha kumekuwa na ongezeko la viongozi wanaowasilisha fomu za Tamko kwa wakati.

Kwa upande wa uhakiki wa Taarifa za Mali na Madeni ya Viongozi wa Umma, katika mwaka huu wa utekelezaji, Tume ya Maadili imewafanyia uhakiki viongozi 168 ikilinganishwa na viongozi 103 katika 2017/18 na viongozi 38 katika mwaka 2016/17. Viongozi hao walikuwa katika ngazi ya uteuzi wa Rais, Mawaziri na Viongozi wa ngazi nyengine kwa mujibu wa nyadhifa zao. Moja kati ya tatizo linaloendelea kujitokeza ni kwa baadhi ya viongozi waliohakikiwa kutokamilisha au kufanya uhaulishaji wa mali walizoziuza au walizozinunua kutoka kwa watu wengine. Hali hii inatoa mwanya wa uwezekano wa kutokuwepo au kupatikana kwa taarifa sahihi za mali na madeni ya viongozi hao.

Tume ya Maadili imeendelea kupokea malalamiko na taarifa za uvunjaji wa maadili kutoka kwa wananchi. Katika mwaka huu wa utekelezaji, malalamiko 13 yamepokelewa. Malalamiko hayo yamewahusu viongozi katika ngazi ya uteuzi wa Rais, Mawaziri na katika ngazi ya Serikali za Mitaa. Maeneo yaliyolalamikiwa ni pamoja na matumizi mabaya ya madaraka na udhalilishaji wa kijinsia. Malalamiko yote yameendelea kufanyiwa kazi kwa mujibu wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Kadhalika, Tume ya Maadili inayafanyia kazi maelezo na sababu za viongozi waliochelewa kuleta fomu zao kwa wakati.

copy

Vyombo vya habari vya Serikali, binafsi na redio jamii vimeendelea kutumiwa katika kuielimisha jamii kuhusu umuhimu wa viongozi kuzingatia maadili katika utekelezaji wa majukumu yao. Wananchi wameendelea kuelimishwa wajibu wao katika suala hili kwa kupitia makala, vipindi, matangazo na maigizo mbalimbali yaliyoandaliwa na kurushwa au kuchapishwa katika vyombo hivyo vya habari.

Kwa mara ya kwanza, maadhimisho ya Siku ya Maadili na Haki za Binaadam yalifanyika katika kiwanja cha Gombani, Chake Chake Pemba. Makamo wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Mhe. Balozi Seif Ali Iddi alimwakilisha Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein kuwa mgeni rasmi katika sherehe hizo. Katika kilele cha maadhimisho ya siku ya Maadili, taaasi za utawala bora ziliandaa programu mbalimbali kwa lengo la kuimarisha utawala bora nchini kupitia elimu ya maadili, mapambano dhidi ya rushwa, haki za binadamu, matumizi mabaya ya rasilimali za serikali, uwazi na uwajibikaji.

copy

Nimalizie kwa kuanza kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohamed Shein, kwa jitihada zake za kuimarisha Utawala Bora nchini kwa kuhimiza uwajibikaji na kuimarisha maadili na kuanzisha taasisi za kusimamia utawala bora, ikiwemo Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Aidha, ninamshukuru Makamu wa Pili wa Rais, Mhe. Balozi Seif Ali Iddi, kwa kusimamia vyema utendaji wa shughuli za Serikali katika kuhakikisha malengo yaliyowekwa yanafikiwa.

Pili, ninapenda kumshukuru Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Haroun Ali Suleiman, pamoja na viongozi wote wa Wizara kwa mwongozo, ushauri na msaada waliotupatia katika

kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Tume ya Maadili.

Kadhalika, ninawashukuru kwa dhati Makamishna wa Tume ya Maadili, Mhe. Sebtuu Mohammed Nassor na Mhe. Said Bakari Jecha, pamoja na watendaji wote wa Tume ya Maadili kutokana na utendaji wao uliotuwezesha kupata mafanikio tuliyoyafikia. Makamishna hao wamemaliza kipindi chao cha kwanza tarehe 24 Julai, 2019 na kuteuliwa tena kwa kipindi chengine cha miaka mitatu kuanzia tarehe 25 Julai, 2019. Makamishna hao wameisaidia sana Tume ya Maadili katika kuijenga na kuiimarisha kama taasisi na kupelekea kupata mafanikio iliyofikia. Aidha, katika kipindi hiki cha utekelezaji kulitokea mabadiliko ya uongozi katika Tume ya Maadili. Nd. Asma Hamid Jidawy aliteuliwa kuwa Katibu mpya wa Tume ya Maadili kuanzia tarehe 12 Novemba, 2018.

copy

Mwisho, ninapenda kutoa wito kwa Viongozi wa Umma na Wananchi wote waendelee kutoa ushirikiano ili kwa pamoja tuiwezeshe Tume ya Maadili kufikia malengo ya kuanzishwa kwake katika kuimarisha Utawala Bora.

Kwa heshima, naomba kuwasilisha.

**Assaa Ahmad Rashid**

**Mwenyekiti**
**Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma**

***'Fuata Maadili, Tuimarishe Utawala Bora'.***

## 1.0 UTANGULIZI

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imepitisha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Nam. 4 ya 2015 inayoweka viwango vya maadili kwa viongozi wa umma ambavyo wanapaswa kuvizingatia wakati wa utekelezaji wa majukumu yao kwa umma. Sheria hiyo imeanzisha Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma (Tume ya Maadili) ambayo imepewa jukumu la kuisimamia kwa lengo la kuimarisha maadili kwa viongozi wa umma.

Kupitishwa kwa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, ni sehemu ya juhudi za Serikali katika kuimarisha utawala bora nchini. Miongoni mwa taasisi nyengine zilizoanzishwa na Serikali kwa lengo hilo ni pamoja na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi pamoja na Idara ya Utawala Bora.

copy

Ripoti hii inaelezea utekelezaji wa majukumu ya Tume ya Maadili katika kusimamia shughuli zake za masuala ya maadili. Utekelezaji huu ni kwa mujibu wa Mpangokazi wa Tume ya Maadili wa 2018/2019, Mipango Mikuu ya Kitaifa ikijumuisha Dira ya Maendeleo ya 2020, MKUZA na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2015-2020.

### 1.1 DIRA

Dira ya Tume ya Maadili ni *"Kuwa na jamii yenye kufuata maadili"*

### 1.2 DHAMIRA

Dhamira ya Tume ya Maadili ni *"Kukuza tabia na vitendo vyenye*

*kufuata maadili kwa Viongozi wa umma kwa kuimarisha uwazi, uwajibikaji, utii na usimamizi wa sheria".*

## 1.3 MAADILI YA MSINGI

Utendaji kazi wa Tume ya Maadili umejengwa kwa kuzingatia misingi ya maadili ifuatayo ambayo inawaongoza watumishi wake:

(a) **Uadilifu:** Kufanya kazi kwa uwazi na bila ya upendeleo;

(b) **Usiri:** kuhifadhi na kutunza taarifa zote za siri ikiwemo taarifa zinazohusiana na mali na madeni ya Viongozi wa Umma;

(c) **Utaalamu:** Kusimamia sheria ya Maadili ya Viongozi kwa umakini na uaminifu kwa kutumia umahiri, uweledi, na utaalamu unaohitajika;

(d) **Uwajibikaji:** Kuimarisha uwajibikaji wa watumishi na wahusika wengine wa Tume; na

(e) **Kufanya kazi kwa mashirikiano:** Kukuza na kuimarisha ushirikiano miongoni mwa watumishi ili kuwezesha utendaji wa kazi za Tume kwa ufanisi.

## 1.4 LENGO KUU

Lengo kuu la Tume ya Maadili ni *"Kusimamia maadili ya Viongozi wa Umma Zanzibar"*

## 2.0 MUUNDO WA TUME YA MAADILI

Kwa mujibu wa Kifungu cha 5(1) cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Tume ya Maadili inaundwa na Mwenyekiti na Makamishna wawili (wa muda) ambao wanateuliwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Kwa mujibu wa kifungu cha 5(2) cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Mwenyekiti anasimamia kazi na anatekeleza majukumu na mamlaka ya Tume ya Maadili. Kadhalika, Tume ya Maadili ina Katibu ambaye anateuliwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Katibu wa Tume anasimamia kazi za kiutawala za kila siku na anawajibika kwa Tume. Kadhalika, Tume ya Maadili ina Afisa Mdhamini ambaye anaratibu shughuli za Tume ya Maadili kwa upande wa Ofisi ya Tume ya Maadili, Pemba. Aidha, Tume ya Maadili ina watumishi wa fani nyengine tofauti kwa kuzingatia muundo wake kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma. Muundo wa Tume ya Maadili ni kama unavyoonekana kwenye ***Kiambatanisho Nambari 1***.

copy

## 2.1 IDARA ZA TUME YA MAADILI

Tume ya Maadili ina Idara mbili; Idara ya Maadili ya Viongozi na Idara ya Mipango, Utawala na Rasilimali Watu pamoja na Ofisi ya Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Pemba. Idara ya Maadili ya Viongozi inajumuisha Sehemu ya Usajili na Kumbukumbu na Sehemu ya Maadili na Uchunguzi. Idara ya Mipango, Utawala na Rasilimali Watu inajumuisha sehemu ya Utawala na Rasilimali Watu na Sehemu ya Mipango, Sera na Utafiti. Aidha, Tume ya Maadili ina vitengo vitano ambavyo ni: Fedha na Uhasibu, Huduma za Sheria, Uhusiano na Elimu kwa Umma, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano na Kitengo cha Ununuzi. Ofisi ya Tume ya Maadili Pemba inajumuisha sehemu ya Usajili na Kumbukumbu na sehemu ya Maadili na Uchunguzi.

copy

## 2.2 WATUMISHI WA TUME YA MAADILI

Katika kipindi hiki cha utekelezaji, Tume ya Maadili ina watumishi 20 ambao wako katika fani za Sheria, Mipango, Utunzaji wa kumbukumbu, Utumishi, Utawala, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, Uhusiano na Elimu kwa Umma, Ununuzi na Uhasibu. Kati ya watumishi hao 20, watumishi 11 ni wanawake na 9 ni wanaume. Awali, watumishi wa Tume ya Maadili walikuwa 21 kabla ya mtumishi mmoja kupata uteuzi wa kuwa Msaidizi Mkurugenzi Wilaya ya Magharibi A. Baada ya kuidhinishwa rasmi muundo wa Tume ya Maadili, watumishi wengine 11 wenye uzoefu na fani zinazoendana na mahitaji ya Tume ya Maadili kwa mujibu wa muundo huo, wataongezwa katika mwaka wa fedha unaofuata, 2019/2020 ili kuongeza kasi ya utendaji na ufuatiliaji. Idadi ya Watumishi na viwango vyao vya elimu ni kama inavyoonekana katika ***Jadweli Nambari 1.***

copy

**Jadweli Nambari 1: Idadi ya Watumishi wa Tume ya Maadili na Viwango vyao vya Elimu.**

| CHETI/ FORM II-VI | | STASHAHADA | | STASHA HADA YA JUU | | SHAHADA | | STASHAH ADA YA UZAMILI | | SHAHADA YA UZAMILI | | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| KE | ME | KE | ME | KE | ME | KE | ME | KE | ME | KE | ME | |
| 1 | 3 | 4 | - | 0 | 0 | 4 | 1 | 1 | 1 | 1 | 4 | **20** |

## 2.3 MAJUKUMU YA TUME YA MAADILI

Kwa mujibu wa kifungu cha 12(1) cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Tume ya Maadili ina majukumu yafuatayo:

(a) Kupokea na kuhifadhi Tamko la Mali na Madeni ambalo limetolewa na Kiongozi wa Umma;

(b) Kupokea tuhuma na taarifa za uvunjaji wa maadili kutoka kwa wananchi;

copy

(c) Kufanya uchunguzi juu ya madai au tuhuma za uvunjaji wa maadili kwa kiongozi yeyote wa Umma;

(d) Kupokea, kuchunguza na kushughulikia madai yote yanayohusu uvunjaji wa maadili katika chombo cha umma;

(e) Kupokea na kuchunguza jambo lolote ambalo kwa maoni ya Tume linapelekea tuhuma ya moja ya mambo yafuatayo kuwa limetokea au linaweza kutokea:

(i) Kitendo kinachopelekea uvunjaji wa maadili;

(ii) Kitendo kinachopelekea kuruhusu, kushawishi au kusababisha uvunjaji wa maadili;

(f) Kuchunguza mwenendo wa kiongozi yeyote wa umma ambao kwa maoni ya Tume, unapelekea au unachangia uvunjaji wa maadili;

(g) Kusikiliza na kutoa maamuzi kuhusu madai yoyote ya uvunjaji wa Maadili dhidi ya Kiongozi wa Umma;

(h) Kutoa uamuzi wa uvunjaji wowote wa maadili;

(i) Kusaidia taasisi yoyote ya Serikali yenye jukumu la kutekeleza Sheria katika kufanya uchunguzi wa kosa la uvunjaji wa maadili;

(j) Kutokana na maombi ya mtu au taasisi yoyote, kushauri au kusaidia mtu au taasisi yoyote namna ambavyo kiongozi au taasisi hiyo inavyoweza kuepukana na uvunjaji wa maadili;

copy

(k) Kuelimisha umma juu ya umuhimu wa maadili;

(l) Kufanya uchunguzi juu ya jambo lolote ambalo kwa maoni ya Tume linastahili kufanyiwa uchunguzi;

(m) Kutoa ushauri, maelekezo na miongozo kuhusiana na maadili ya Viongozi;

(n) Kufanya uhakiki wa moja kwa moja kuhusiana na Tamko la Mali na Madeni lililowasilishwa kwa mujibu wa sheria; na

(o) Kufanya kazi nyengine zozote ilizopewa na Sheria ya Maadili ya

Viongozi au Sheria nyenginezo.

## 2.4 MAMLAKA NA UWEZO WA TUME YA MAADILI

Katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu yake, Tume ya Maadili imepewa mamlaka na uwezo wa:

(a) Kumuidhinisha afisa wa Tume kufanya uchunguzi wa tuhuma ya uvunjaji wa maadili (kif. 13(1)(a)).

(b) Kumtaka mtu yeyote kutoa kumbukumbu na nyaraka zozote zinazohusiana na tuhuma zinazofanyiwa uchunguzi (kif. 13(1)(b)).

(c) Kumtaka mtu yeyote kufika mbele ya Tume kwa ajili ya kuhojiwa kuhusiana na jambo lolote linaloshughulikiwa na Tume katika uchunguzi wa tuhuma za uvunjaji wa maadili (kif.13(1)(c)).

(d) Kumtaka Kiongozi wa Umma kutoa taarifa au maelezo ya ziada kuhusiana na Tamko la Mali na Madeni alililoliwasilisha (kif.16A).

(e) Kushirikiana na taasisi au mtu yeyote katika uchunguzi wa madai au tuhuma za uvunjaji wa Sheria ya Maadili (kif. 14(1)).

(f) Kuchunguza Akaunti ya Kiongozi wa Umma (kif.37(1)).

(g) Kuwasilisha maamuzi yake kwenye mamlaka husika (kif. 27(1)).

copy

## 3.0 KAZI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KWA MWAKA 2018/19

Katika kipindi cha mwaka 2018/2019 kazi zilizopangwa kutekelezwa ni kama ifuatavyo: -

(a) Kupokea na kusajili Taarifa za Mali na Madeni ya Viongozi wa Umma;

(b) Kuandaa Mfumo wa Kielektroniki wa Usajili wa Taarifa za Mali na Madeni ya Viongozi wa Umma;

(c) Kufanya uhakiki wa Taarifa za Mali na Madeni kwa Viongozi wa Umma;

(d) Kupokea na kufanya uchunguzi wa tuhuma na malalamiko ya ukiukaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma;

(e) Kujenga uelewa kwa Wananchi na Viongozi wa Umma Unguja na Pemba kuhusu umuhimu wa Maadili ya Viongozi wa Umma;

(f) Kuadhimisha siku ya Maadili na Haki za Binadamu;

(g) Kuwapatia mafunzo ya kitaalam Watumishi wa Tume ya Maadili;

(h) Kukamilisha Mpango Mkakati wa Tume ya Maadili; na

(i) Kukuza na kuimarisha ushirikiano na uhusiano Kitaifa, Kikanda na Kimataifa.

## 4.0 UTEKELEZAJI HALISI WA KAZI ZA TUME YA MAADILI KWA MWAKA 2018/2019

Katika mwaka huu wa utekelezaji, Tume ya Maadili imeweza kutekeleza kazi zake kama ifuatavyo: -

### 4.1 TAMKO LA MALI NA MADENI YA VIONGOZI WA UMMA

copy

Kwa mujibu wa kifungu cha 15(1) cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, kila kiongozi wa umma anatakiwa kujaza na kuwasilisha Tume ya Maadili, Fomu ya Tamko la Mali na Madeni. Fomu ya Tamko huwasilishwa kila ifikapo mwezi wa Disemba ya kila mwaka, ndani ya siku thelathini (30) baada ya kiongozi wa umma kushika madaraka au wadhifa wa uongozi na mara tu baada ya kiongozi wa umma kumaliza muda wa kushika madaraka au wadhifa wa uongozi. Orodha ya Viongozi wa Umma, imeelezwa katika Jadweli la Kwanza la Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma. ***Kiambatanisho Nambari 2*** kinahusika.

### 4.1.1 Uchapishaji na Usambazaji wa Fomu ya Tamko la Mali na Madeni

Kwa mwaka 2018/2019, Tume ya Maadili ilichapisha fomu za Tamko la Mali na Madeni 2,300 na kuzisambaza kwa viongozi kupitia mikutano mbalimbali ya viongozi wa umma iliyofanyika Unguja na Pemba. Fomu hizo pia ziliwasilishwa katika makao makuu ya kila Wizara na Taasisi husika ili viongozi waliokuwa hawakuhudhuria mikutano hiyo waweze kuzipata kwa urahisi. Kadhalika, fomu hizo zilipatikana katika tovuti ya Tume ya Maadili **www.ethicscommission.go.tz** ambapo baadhi ya viongozi waliweza kuzipata kupitia tovuti hiyo, kuzijaza na kuziwasilisha katika ofisi za Tume ya Maadili Unguja na Pemba. Matarajio ya Tume ya Maadili ni kuendelea kuwaomba viongozi wa umma watumie njia ya kupata fomu kupitia tovuti ya Tume ya Maadili ili Serikali iweze kupunguza gharama za uchapishaji na usambazaji wa Fomu za Tamko la Mali na Madeni.

copy

### 4.1.2 Uchambuzi wa Fomu

Kwa mwaka 2018/19 Tume ya Maadili ilikadiria kupokea jumla ya fomu 1,650 ambapo hadi kufikia tarehe 31 Disemba, 2018 jumla ya fomu 1,649 zilipokelewa. Hata hivyo, Tume ya Maadili ilieendelea kupokea fomu kutoka kwa viongozi waliochelewa na waliopata uteuzi

mpya baada ya tarehe 31 Disemba 2018. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2019 Tume ya Maadili ilipokea jumla ya fomu za viongozi 1,702 sawa na asilimia 103 ya shabaha ya fomu 1,650. Idadi hiyo ikilinganishwa na fomu zilizopokelewa mwaka uliopita 2017/18 (1,664) ni sawa na asilimia 101.


Aidha, kati ya Fomu hizo (1,702), zilizowasilishwa ndani ya muda ni 1,676 ukijumuisha na uteuzi mpya wa viongozi 27 (ikilinganishwa na 1,639 za mwaka 2017/18). Viongozi waliowasilisha fomu nje ya muda ni 26, ikilinganishwa na viongozi 25 kwa mwaka 2017/18. Muhtasari wa uwasilishaji wa fomu kiidadi ni kama unavyoonekana katika ***Jadweli Nambari 2 na Mchoro Nambari 1.***

**Jadweli Nambari 2: Muhtasari wa Uwasilishaji wa Fomu**

| **MAELEZO** | **2016/2017** | **2017/2018** | **2018/2019** |
|---|---|---|---|
| MAKADIRIO | 1600 | 1650 | 1650 |
| FOMU ZILIZOWASILISHWA | 1620 | 1664 | 1702 |
| ZIADA/UPUNGUFU | 20 | 14 | 52 |
| ASILIMIA - UWASILISHAJI | 101 | 101 | 103 |
| NDANI YA MUDA | 1,479 | 1,639 | 1676 |
| WALIOCHELEWA | 141 | 25 | 26 |
| ASILIMIA -WALIOCHELEWA | 9 | 2 | 2 |

copy

**Mchoro Nambari 1: Muhtasari wa Uwasilishaji wa Fomu**




Kwa mujibu wa kifungu cha 16A(1) cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Tume ya Maadili inaweza kumtaka kiongozi yeyote wa umma kutoa taarifa au maelezo ya ziada kuhusiana na Tamko la Mali na Madeni alilowasilisha. Katika mwaka huu wa utekelezaji, jumla ya viongozi 47 walitakiwa kutoa taarifa za ziada kuhusiana na taarifa zao za mali na madeni.

### 4.1.3 Kutangaza Majina ya Viongozi wa Umma katika Gazeti Rasmi la Serikali

Kwa mujibu wa Kifungu cha 22(3) cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, majina ya Viongozi wa Umma waliowasilisha fomu yalichapishwa katika Gazeti Rasmi la Serikali katika Tangazo la Kisheria Nambari 6 la Mwaka 2019. Majina hayo yanajumuisha Viongozi wa Umma waliowasilisha Fomu zao hadi tarehe 26 Januari, 2019. Aidha, majina ya viongozi wengine huchapishwa baada ya kuwasilisha fomu zao kutokana na teuzi mpya au kuchelewa kuwasilisha fomu zao.

copy

### 4.1.4 Ufuatiliaji na Ukusanyaji wa Taarifa za Viongozi Wasiojaza Fomu

Katika kuimarisha Daftari la Usajili wa taarifa za viongozi, Tume ya Maadili iliunda kikundi kazi maalum kwa ajili ya kubaini na kujiridhisha juu ya kuwepo au kutokuwepo kwa Viongozi wa Umma wengine ambao wanaostahiki kujaza Fomu ya Tamko la Mali na Madeni. Kazi hiyo ilifanyika kwa kuzitembelea taasisi zote za serikali kwa lengo la kufanya uhakiki wa kubaini na kuwatambua viongozi ambao wanawajibika kujaza fomu kwa mujibu wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma lakini hawatekelezi wajibu huo.

Aidha, kazi hii ilihusisha kuwatambua Viongozi ambao tayari wameshaondoka katika nyadhifa zao, wastaafu na wale ambao wameshafariki. Uchambuzi wa kina unaendelea ili kubaini viongozi wanaostahiki kujaza Fomu ya Tamko la Mali na Madeni. Miongoni mwa viongozi hao inajumuisha wateule wa mawaziri na wahasibu. Kazi hii inatarajiwa kukamilika katika mwaka 2019/2020. Hata hivyo, idadi ya viongozi wanaowajibika kujaza fomu inaweza kuongezeka, kwa kuwa orodha ya viongozi inayofanyiwa kazi hadi sasa inahusisha viongozi 318.

copy

## 4.2 MFUMO WA KIELEKTRONIKI WA KUSAJILI TAARIFA ZA MALI NA MADENI YA VIONGOZI WA UMMA

Katika kuimarisha mazingira bora ya utendaji wa kazi katika mwaka huu wa utekelezaji, Tume ya Maadili imeendelea kuandaa mfumo wa kielekroniki kwa ajili ya usajili wa Taarifa za Mali na Madeni ya Viongozi wa Umma. Mfumo huo unategemewa kuanza kutumika katika mwaka 2019/2020. Kazi ya uingizaji wa Taarifa za Mali na Madeni ya viongozi imeanza kwa majaribio ili kuhakikisha kuwa taarifa rasmi zikiingizwa kusijitokeze hitilafu yoyote.

Taarifa hizo za viongozi zitaimarishwa kwa kuingiza taarifa zao za ziada zitakazojitokeza kutokana na mabadiliko ya taarifa za viongozi wanaohusika, kutokana na sababu za uteuzi, kustaafu, kumaliza muda na mabadiliko ya nafasi za uongozi.

Kukamilika kwa mfumo huo, kutaiwezesha Tume ya Maadili kuhifadhi taarifa za viongozi kwa ufanisi zaidi na hivyo kurahisisha utekelezaji wa majukumu yake katika uandaaji wa ripoti na taarifa, uchunguzi, uhakiki na utoaji wa takwimu zinazohusiana na taarifa za viongozi wa umma. Kazi ya uandaaji wa Mfumo wa Kielektroniki wa Usajili wa Taarifa za Mali na Madeni inatekelezwa kwa ushirikiano baina ya watendaji wa Tume ya Maadili katika Kitengo cha TEHAMA na Idara ya Serikali Mtandao.

copy

## 4.3 UHAKIKI WA TAARIFA ZA MALI NA MADENI YA VIONGOZI WA UMMA

Kwa mujibu wa kifungu cha 12(1)(n) cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Tume ya Maadili inatakiwa kufanya uhakiki wa taarifa za Mali na Madeni ya Viongozi wa Umma zilizojazwa kwenye Fomu ya Tamko la Mali na Madeni.

Jukumu hili la uhakiki hutekelezwa baada ya Viongozi wa Umma kuwasilisha Fomu zao za Tamko la Mali na Madeni, ili Tume ya Maadili iweze kujiridhisha na usahihi wa taarifa zilizotolewa. Tume ya Maadili inaweza kumtaka kiongozi wa umma kutoa taarifa au maelezo ya ziada kuhusiana na Tamko la Mali na Madeni wakati wa uhakiki.

### 4.3.1 Uchambuzi wa Taarifa za Uhakiki

Uchambuzi wa taarifa za uhakiki unazingatia vigezo mbalimbali vya

matakwa ya Sheria ya Maadili, ikiwemo nafasi au cheo cha kiongozi, malalamiko, madai au tuhuma zilizowasilishwa kuhusu Kiongozi husika. Aidha, uhakiki unazingatia usahihi wa ujazaji wa Tamko la Mali na Madeni na uwezekano wa kiongozi kuingia katika mgongano wa maslahi.

Kwa mwaka huu wa utekelezaji 2018/2019, Tume ya Maadili ilipanga kuhakiki jumla ya Viongozi 120 ambapo hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2019 Jumla ya Viongozi 168 wamehakikiwa Unguja na Pemba sawa na asilimia 140. Ikilinganishwa na mwaka uliopita 2017/2018, Tume ya Maadili ilipanga kuwafanyia uhakiki jumla ya Viongozi 360 ambapo utekelezaji halisi ni 103 sawa na asilimia 29. Kwa mwaka huu wa utekelezaji 2018/2019 kuna ongezeko la Viongozi 65 waliofanyiwa uhakiki kutoka Viongozi 103 (2017/2018) hadi 168 (2018/2019). ***(Angalia Jadweli Nambari 3 na Mchoro Nambari 2*** inahusika*)*. Hali hii imetokana na kuongezeka kwa bajeti ya Tume ya Maadili na vitendea kazi, kuongezeka na kuimarika kwa uzoefu na utaalamu kwa watumishi wa Tume ya Maadili.


copy

Aidha, kwa mwaka ujao wa fedha 2019/2020 Tume ya Maadili imepanga kuhakiki Viongozi wa Umma 220, sawa na ongezeko la viongozi 100 ikilinganishwa na lengo la mwaka 2018/19.

**Jadweli Nambari 3: Uhakiki kwa Viongozi wa Umma kwa mwaka 2018/2019**

| **MWAKA** | **VIONGOZI WALIOPANGWA KUHAKIKIWA** | **UTEKELEZAJI HALISI** | **ASILIMIA** |
|---|---|---|---|
| 2016/2017 | 56 | 38 | 68 |
| 2017/2018 | 360 | 103 | 29 |
| 2018/2019 | 120 | 168 | 140 |
| 2019/2020 | 220 | - | - |

**Mchoro Nambari 2: Uhakiki kwa Viongozi wa Umma kwa mwaka 2018/2019**




Katika mwaka huu wa utekelezaji 2018/19, Viongozi waliofanyiwa uhakiki ni baadhi ya Mawaziri na Naibu Waziri, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, Naibu Katibu Mkuu, Mahakimu wa Mkoa na Wilaya, Wakurugenzi wa Idara za Uendeshaji na Utumishi na Wakurugenzi wa Idara za Mipango, Sera na Utafiti. Orodha hiyo pia ilijumuisha baadhi ya Wakurugenzi katika Idara, Mashirika na Taasisi za Wizara, Wahasibu na Wakaguzi wa ndani wa Hesabu za Serikali, pamoja na viongozi wengine katika ngazi ya Serikali za Mitaa.

copy

Hata hivyo, baadhi ya Viongozi waliohakikiwa wamebainika kuwa hawajafanya au hawajakamilisha taratibu za uhaulishaji wa mali zao zinazohamishika na zisizohamishika. Hivyo, walishindwa kuwasilisha nyaraka za mali wanazozimiliki kwa majina yao kama vile kadi za umiliki wa vyombo vya moto, hatimiliki za nyumba, majengo, mashamba, viwanja, mashine na mitambo. Hali hii inaweza kupelekea baadhi ya mali za viongozi hao kutokuorodheshwa katika Fomu ya Tamko la Mali na Madeni au kutokutambulika kwa mali halisi za viongozi husika, na hivyo kukosekana kwa kumbukumbu sahihi za taarifa za mali zao katika Daftari la Usajili.

Kwa mwaka 2018/2019 viongozi waliopangiwa kufanyiwa uhakiki walikuwa na mali Unguja, Pemba na nje ya Zanzibar. Kati ya viongozi 168 waliofanyiwa uhakiki, Viongozi 11 wameeleza wanamiliki mali Unguja, Pemba na nje ya Zanzibar. Mali zilizopo nje ya Zanzibar za viongozi 11 zimepangwa kufanyiwa uhakiki katika mwaka wa fedha 2019/2020.

### 4.3.2 Mgongano wa Kimaslahi

Katika uhakiki uliofanyika mwaka 2018/2019, imeonekana kuna uwezekano kwa baadhi ya Viongozi wa Umma kuingia katika mgongano wa kimaslahi ambao unaweza kupelekea kuathiri utekelezaji wa kazi au majukumu yao kwa umma. Miongoni mwa maeneo ambayo mgongano wa kimaslahi unaweza kujitokeza ni pamoja na umiliki wa hisa katika kampuni za biashara za ukandarasi, hoteli, mikahawa, ununuzi na usambazaji wa bidhaa na huduma pamoja na utoaji ushauri wa kitaalamu.

copy

Tume ya Maadili inaendelea kufuatilia ili kuweza kubaini kama mgongano huu unapelekea kuvunja Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma na kuchukua hatua zinazostahiki. Aidha, Tume ya Maadili inaendelea kutoa elimu ya maadili, ikiwemo athari ya mgongano wa kimaslahi, ili viongozi wa umma waweze kuzingatia maadili na miiko ya uongozi kwa kudhibiti na kuepuka kuingia katika mgongano wa maslahi katika utekelezaji wa majukumu yao.

## 5.0 KUPOKEA NA KUFANYA UCHUNGUZI WA TUHUMA NA MALALAMIKO YA UKIUKWAJI WA SHERIA YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA

Kifungu cha 12(1)(b)-(f) cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, kinaipa Tume ya Maadili uwezo wa kupokea na kufanya uchunguzi kuhusu malalamiko, tuhuma, madai au taarifa za ukiukwaji wa maadili

ya Viongozi.

Katika kipindi cha mwaka 2018/2019, Tume ya Maadili ilipokea na kuyashughulikia jumla ya malalamiko 13 dhidi ya Viongozi wa Umma, ikilinganishwa na malalamiko 6 katika mwaka 2017/18. Malalamiko hayo yalihusu maeneo mbalimbali ikiwemo matumizi mabaya ya madaraka, udhalilishaji wa kijinsia, ubadhirifu wa mali za umma, kashfa na matumizi ya lugha ya matusi na upendeleo katika ajira. ***Jadweli Nambari 4*** inahusika.

**Jadweli Nambari 4: Idadi ya Malalamiko iliyopokelewa na Tume 2018/2019**

| S/N | Malalamiko | 2016/17 | 2017/2018 | 2018/2019 |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Malalamiko yanayohusu Tume | 3 | 6 | 10 |
| 2 | Malalamiko yaliyopelekwa Taasisi nyengine (ZAECA, DPP) | 1 | 0 | 3 |
| | **Jumla ya Malalamiko yaliopokelewa** | **4** | **6** | **13** |

copy

## 5.1 Uchambuzi wa Malalamiko

Kati ya malalamiko mawili ya udhalilishaji wa kijinsia yaliyopokelewa, lalamiko moja limepelekwa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa kuwa lilihusika na tuhuma za makosa ya kijinai. Aidha, Tume ya Maadili inasubiri maamuzi ya kesi inayohusu lalamiko jengine la udhalilishaji kwa kuwa kiongozi wa umma anayelalamikiwa ameshafikishwa katika vyombo vya Sheria. Kadhalika, kiongozi mwengine wa umma anayelalamikiwa kwa matumizi mabaya ya madaraka amefunguliwa kesi ya madai na mlalamikaji inayohusu mgogoro wa matumizi ya ardhi.

Kwa mujibu wa kifungu cha 22(2) cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Tume ya Maadili inatakiwa kufanya uchunguzi wa awali

kuhusu malalamiko na madai yaliyowasilishwa. Iwapo Tume ya Maadili itaridhika kuwa uchunguzi unaonesha kuna hoja za kujibiwa na kiongozi wa umma, itamtaka kiongozi huyo kutoa maelezo kwa maandishi kuhusu madai au malalamiko hayo. Katika uchunguzi wa awali kuhusu malalamiko yaliyowasilishwa, Tume ya Maadili ilibaini kuwa malalamiko 3 hayakuwa na hoja za msingi za kutaka kujibiwa na viongozi wa umma.

Katika uchunguzi wa awali kuhusu malalamiko 7 yaliyowasilishwa, Tume ya Maadili imebaini kuwa uchunguzi unaonesha kuwa kuna hoja za kujibiwa na viongozi wa umma wanaolalamikiwa. Hivyo, viongozi hao walipewa muda wa siku 14 na kutakiwa kutoa maelezo ya maandishi kuhusu madai hayo. Maelezo ya viongozi hao yameshawasilishwa Tume ya Maadili na yameshafanyiwa uchambuzi ili kubaini hatua nyengine zinazopaswa kuchukuliwa. Matokeo ya uchambuzi wa maelezo yao umebaini kuwa viongozi 2 watatakiwa kuitwa mbele ya Tume ya Maadili kwa ajili ya kusikiliza malalamiko au madai yaliyowasilishwa dhidi yao. Uchunguzi na ukusanyaji wa taarifa za ziada unaendelea kwa malalamiko mengine 5 yaliyobakia. Kada zilizolalamikiwa zinawahusisha watendaji wakuu wa Wizara, Idara na Taasisi za SMZ, Wateule wa Mawaziri na Viongozi wa Serikali za Mitaa. Mchanganuo unaonekana katika ***Kiambatanisho Nambari 3*** *kinahusika.*

Tume ya Maadili inaendelea kutoa elimu kwa umma na hasa kwa Viongozi ili kupunguza malalamiko yasiyo na msingi hasa yale ya ukiukwaji wa Sheria dhidi ya Maadili ya Viongozi wa Umma.

## 6.0 KUJENGA UELEWA KWA WANANCHI NA VIONGOZI WA UMMA UNGUJA NA PEMBA KUHUSU MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA

Kifungu cha 12(1)(k) cha Sheria ya Maadili kimeipa Tume ya Maadili wajibu wa kutoa elimu kuhusu umuhimu wa Maadili ya viongozi wa

copy

umma. Katika kuwapatia elimu hiyo Viongozi wa umma, watumishi wa umma na wananchi kwa ujumla, Tume ya Maadili imetumia njia mbalimbali ili kuongeza uelewa juu ya umuhimu wa maadili ya viongozi wa umma katika kuimarisha utawala bora na ustawi wa jamii.

Tume ya Maadili iliandaa na kufanya mikutano ya utoaji wa elimu kwa viongozi wa umma, watumishi wa umma na wananchi. Aidha, vipeperushi na machapisho vilitayarishwa na kusambazwa. Kadhalika, vipindi vya elimu na matangazo kupitia vyombo mbalimbali vya habari vilitayarishwa na kurushwa hewani, ***Jadweli Nambari 5*** *inahusika.*

### 6.1 Mikutano na Viongozi wa Umma

Katika mwaka 2018/2019, Tume ya Maadili iliweka shabaha ya kufanya mikutano 30 ya viongozi wa umma katika Wizara, Idara, Mashirika na Taasisi za Umma. Jumla ya mikutano 30 ilifanyika, kati ya hiyo Unguja 23 na Pemba 7. Mada zilizowasilishwa katika mikutano hiyo ni:

a) Umuhimu wa Maadili kwa Viongozi wa Umma;
b) Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Nam. 4 ya 2015 na marekebisho yake; na
c) Ujazaji wa Fomu ya Tamko la Mali na Madeni.

### 6.2. Mikutano na Wananchi na Wanafunzi

Katika kipindi hiki cha utekelezaji kwa mwaka 2018/2019, Tume ya Maadili ilifanya mikutano na wananchi pamoja na makundi mbalimbali. Miongoni mwa wananchi waliopata elimu hii ni pamoja na wananchi wa Shehia ya Kilindi na Tumbe Mashariki Pemba. Kadhalika, elimu ya maadili imetolewa kwa wanafunzi wa Skuli 3 za Uzini Unguja, Kilindi na Mzambarau Takau Pemba.

copy

Aidha, Tume ya Maadili iliandaa na kufanya mikutano 7 na Mabaraza ya Vijana Unguja na Pemba. Kwa upande wa Unguja mikutano 5 imefanyika na Mabaraza ya Vijana ya Wilaya ya Kaskazini A, Wilaya ya Kaskazini B, Wilaya ya Kati na Wilaya ya Kusini. Wilaya ya Mjini, Wilaya ya Magharibi A na Wilaya ya Magharibi B zilifanyiwa mkutano kwa pamoja. Kwa upande wa Pemba, mikutano 2 ilifanyika na kuwahusisha Wajumbe wa Mabaraza ya Vijana ya Wilaya za Mkoani, Chake Chake, Micheweni na Wete. Lengo la mikutano hiyo ni kuitambulisha Tume ya Maadili na kutoa elimu ya maadili kwa wajumbe wa Mabaraza hayo. Mada mbili zilizowasilishwa katika mikutano hiyo ni:

a) Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Nam. 4 ya 2015; na
b) Nafasi ya Mabaraza ya Vijana katika kuimarisha Maadili.

copy

**Jadweli Nambari 5: Mikutano ya Viongozi, Wananchi na Mabaraza ya Vijana waliopatiwa Elimu ya Kukuza Maadili**

| Nam. | AINA YA KUNDI | IDADI YA MIKUTANO | MAENEO |
|---|---|---|---|
| 1 | Mikutano ya Viongozi na Watumishi wa Umma | 30 | Wizara, Idara, Mashirika na Taasisi za Umma |
| 2 | Mikutano ya Wananchi na Wanafunzi | 5 | Shehia ya Kilindi na Tumbe Mashariki; Skuli za Uzini, Kilindi na Mzambarau Takau |
| 3 | Mikutano saba ya Mabaraza ya Vijana | 7 | Wilaya Zote Unguja na Pemba |

## 6.3 Utayarishaji na Urushaji wa Vipindi vya Elimu na Matangazo kupitia Vyombo vya Habari

Katika kipindi hiki cha utekelezaji kwa mwaka 2018/2019, vyombo vya

habari vilitumika kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wa maadili. Vipindi 35 vimetayarishwa na kurushwa hewani kupitia vituo mbalimbali vya Redio na Televisheni. Vituo vilivyotumika kurusha vipindi hivyo ni Shirika la Utangazaji la Zanzibar (ZBC) - Redio na Televisheni, Redio Istiqama na Redio jamii ya Micheweni.

Mada zilizozungumzwa katika vipindi hivyo ni pamoja na Kazi na Majukumu ya Tume ya Maadili, Wajibu wa Viongozi wa Umma katika Kuimarisha Maadili, Jukumu la Wananchi na Jamii katika Kusimamia na Kuhakikisha Viongozi wanafuata maadili.

### 6.4 Utoaji wa Vipeperushi, Machapisho na Matangazo

Katika juhudi za kuitambulisha Tume ya Maadili kwa umma, kalenda 1,500 na vipeperushi 3,000 vilivyobeba maudhui na ujumbe tofauti vilichapishwa. Vipeperushi na kalenda hizo zilisambazwa katika mikutano mbalimbali, maadhimisho ya Siku ya Maadili na Haki za Binadamu iliyofanyika tarehe 10 Disemba, 2018 na Maadhimisho ya Siku ya Sheria Zanzibar iliyofanyika tarehe 4 Februari, 2019.

Aidha, matangazo mbali mbali yalitolewa kupitia Shirika la Utangazaji la Zanzibar (ZBC) - Redio na Televisheni na kupitia Gazeti la Zanzibar Leo. Matangazo hayo yalilenga kuwakumbusha Viongozi wajibu wao wa kujaza Fomu ya Tamko la Mali na Madeni, na kuielimisha jamii kuhusu majukumu ya viongozi na wajibu wao katika kuimarisha maadili ya viongozi wa umma.

## 7.0 MAADHIMISHO YA SIKU YA MAADILI

Siku ya Maadili na Haki za Binaadamu huadhimishwa kwa kuzingatia siku ya Kupinga Rushwa Duniani (9 Disemba) na siku ya Haki za

copy

Binadamu Duniani (10 Disemba) kila mwaka. Tume ya Maadili kwa kushirikiana na Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi, Idara ya Utawala Bora, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora Zanzibar (Taasisi zinazosimamia Utawala Bora), huadhimisha kwa pamoja Siku ya Maadili na Haki za Binaadamu.

Kwa kuwa hapa Tanzania siku ya tarehe 9 Disemba ni siku ya Uhuru wa Tanganyika, siku ya Maadili na Haki za Binaadamu huadhimishwa kila mwaka ifikapo tarehe 10 Disemba. Lengo kuu la maadhimisho haya ni kuendelea na juhudi za kukuza zaidi Utawala Bora na misingi yake ikiwemo mapambano dhidi ya rushwa, haki za binaadamu, uwajibikaji, uwazi, uadilifu na athari ya mgongano wa maslahi katika kutekeleza majukumu ya umma.

Kwa mwaka huu wa utekelezaji, maadhimisho ya Siku ya Maadili na Haki za Binaadamu Kitaifa, yalifanyika katika Uwanja wa Gombani Mpya, Chake Chake Pemba. Katika wiki ya maadhimisho, Taasisi zinazosimamia Utawala Bora zilitoa elimu kwa umma juu ya umuhimu wa mapambano dhidi ya vitendo vya rushwa, ubadhirifu, matumizi mabaya ya fedha na rasilimali za umma, maadili pamoja na kuheshimu na kulinda haki za binadamu. Elimu hiyo ilitolewa kupitia vipindi vya redio na televisheni, michezo mbali mbali, mikutano ya watendaji na viongozi wa umma, na makongamano yaliyojumuisha asasi za kiraia, sekta binafsi na sekta ya umma Unguja na Pemba.

Maadhimisho ya siku ya Maadili yanasaidia kukuza uelewa na kuongeza hamasa kwa wananchi katika dhana ya maadili, mapambano dhidi ya rushwa, kuimarisha uwajibikaji, uwazi na utawala bora kwa ujumla wake. Kwa kuzingatia kuwa viongozi ni watumishi wa umma na vyeo vyote vya madaraka ni dhamana na vipo kwa ajili ya kuwatumikia wananchi. Mgeni Rasmi katika kilele cha sherehe hiyo alikuwa Makamo

copy

wa Pili wa Rais, Mhe. Balozi Seif Ali Iddi, akimuwakilisha Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt Ali Mohamed Shein. Pia Viongozi wa ngazi mbalimbali na wananchi walihudhuria sherehe za maadhimisho hayo. Kauli Mbiu ya maadhimisho hayo kwa mwaka 2018 ni ***"Tuimarishe Uadilifu, Uwajibikaji, Haki za Binaadamu na Mapambano dhidi ya Rushwa kwa Maendeleo ya Taifa"***.

## 8.0 KUWAPATIA MAFUNZO YA KITAALAM WATUMISHI WA TUME YA MAADILI

Katika kuwajengea uwezo watumishi wa Tume ya Maadili, watumishi wawili wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi ya Maadili, Uongozi na Utawala Bora katika Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere Kampasi ya Dar es Salaam. Aidha, katika maandalizi ya kutumia Mfumo wa Ki-elektroniki utakaotumika katika shughuli za usajili wa taarifa za Viongozi wa Umma, Tume ya Maadili imewapatia watumishi wawili wa Kitengo cha TEHAMA mafunzo mafupi ya 'Network Security'. Lengo la mafunzo hayo ni kuhakikisha usalama wa mfumo wa usajili wa taarifa za mali na madeni mara tu utakapokamilika. Kadhalika, watumishi wengine wawili wa kada ya Utunzaji wa Kumbukumbu wamepatiwa mafunzo mafupi yanayohusiana na Matumizi ya Kompyuta katika Chuo cha "Zanzibar Technology College" na mmoja katika fani ya udereva katika Chuo cha Usafirishaji Dar es Salaam. ***Jadweli Nambari 6*** inahusika.

**Jadweli Nambari 6: Idadi ya Watumishi Waliopatiwa Mafunzo**

| Nam. | Aina ya Mafunzo | Idadi ya Watumishi | Taasisi/Chuo |
|---|---|---|---|
| 1 | Maadili, Uongozi na Utawala Bora | 2 | Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere Kampasi ya Dar es Salaam |
| 2 | Ulinzi wa Mitandao (Network Security) | 2 | "Engo Company Ltd", Dar es Salaam |
| 3 | Utunzaji wa Kumbukumbu | 2 | "Zanzibar Technology College", Zanzibar |
| 4 | Udereva | 1 | Chuo cha Usafirishaji, Dar -es - Salaam |
| | **Jumla** | **7** | |

## 9.0 KUTAYARISHA MPANGO MKAKATI WA TUME YA MAADILI KWA KIPINDI CHA MIAKA MITANO

copy

Rasimu ya awali ya Mpango Mkakati wa Tume ya Maadili inayotoa muongozo katika utekelezaji wa majukumu yake kiufanisi iko katika ngazi za awali za kupata maoni ya wahusika wengine katika ngazi mbalimbali. Kwa kushirikiana na Wataalamu, Tume ya Maadili inaendelea kuhakikisha kuwa kazi hiyo inakamilika katika mwaka wa fedha wa 2019/2020 na kuanza kutumika.

## 10.0 VIKAO VYA TUME

Kwa mujibu wa kifungu cha 12 cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Tume imefanya vikao vya kusikiliza na kutoa maamuzi kuhusu uvunjaji wa Maadili dhidi ya Viongozi wa umma pamoja na vikao vya utekelezaji wa kazi za Tume ya Maadili. Vikao sita (6) vya Tume vimefanyika katika kipindi hiki cha utekelezaji, ambapo vilijadili

mambo mbalimbali kuhusiana na masuala ya Tume ya Maadili na maadili ya viongozi wa umma.

## 11.0 HALI YA UPATIKANAJI WA FEDHA

Kwa mwaka wa fedha uliopita 2017/2018, Tume ya Maadili iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 500,000,000 kwa matumizi ya kawaida ambapo hadi kufikia mwezi Juni, 2018 fedha zilizopatikana ni Shilingi 415,128,963 sawa na asilimia 83.

Katika kipindi hiki cha utekelezaji cha mwaka wa fedha 2018/2019, Tume ya Maadili iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 525,000,000 kwa matumizi ya kawaida ambapo hadi kufikia mwezi Juni, 2019 fedha zilizopatikana ni Shilingi 490,000,000 sawa na asilimia 93. Kadhalika kumekuwa na ongezeko la fedha zilizopatikana kutoka shilingi 415,128,963 hadi 490,000,000 sawa na asilimia 18.


Kwa kulinganisha na mwaka wa fedha uliopita (2017/2018), kumekuwa na ongezeko la bajeti ya Tume ya Maadili kutoka Shilingi 500,000,000 hadi Shilingi 525,000,000 sawa na ongezeko la asilimia 4.8. Hali hiyo imeiwezesha Tume ya Maadili kutekeleza majukumu yake iliyojipangia kwa ufanisi. Muhtasari wa upatikanaji wa fedha ni kama unavyoonekana katika ***Jadweli Nambari 7 na Mchoro Nambari 3***.

copy

**Jadweli Nambari 7: Hali ya Upatikanaji wa Fedha.**

| RUZUKU | MWAKA | KILICHOTENGWA | KILICHOPATIKANA | Asilimia (%) |
|---|---|---|---|---|
| **Matumizi Mengineyo (OC)** | 2017/2018 | 500,000,000 | 415,128,963 | 83 |
| **Matumizi Mengineyo (OC)** | 2018/2019 | 525,000,000 | 490,000,000 | 93 |

**Mchoro Nambari 3: Hali ya Upatikanaji wa Fedha**




## 12.0 VIKWAZO NA UTATUZI WAKE

Katika utekelezaji wa majukumu yake, Tume ya Maadili imepata mafanikio ya kuridhisha. Hata hivyo, kumejitokeza mambo mbalimbali yaliyokwamisha utekelezaji wa kazi za Tume ya Maadili kikamilifu. Baadhi ya mambo hayo na njia zilizotumika kukabiliana nazo ni kama ifuatavyo:

i. Ugumu wa kubaini viongozi wanaoteuliwa na mawaziri mfano wajumbe wa bodi, warajis, n.k. bila ya Tume ya Maadili kupata taarifa za uteuzi huo kutoka kwa baadhi ya Wakuu wa Taasisi; - Jitihada za kuwataka wakuu wa taasisi kutoa taarifa za wateule wa Mawaziri zinaendelea kuchukuliwa.

ii. Kuwepo kwa mkanganyiko katika kada ya uhasibu unaohusisha Msaidizi Mhasibu, Mshika Fedha, Karani Mapato, Afisa Mapato na kusababisha baadhi yao kujihesabu kuwa sio Wahasibu; - Kupitia Kitengo cha Uhusiano na Elimu kwa Umma kwa kushirikiana na Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali, juhudi za kutoa elimu zinaendelea kuchukuliwa.

iii. Uwezekano wa kukosa taarifa sahihi za mali na madeni za viongozi wa umma kutokana na viongozi hao kutokufanya au kutokukamilisha taratibu za uhaulishaji wa mali wanazozimiliki, walizokuwa wanazimiliki au mali wanazozimiliki bila ya kuwa na nyaraka ya aina yoyote; - Tume ya Maadili kwa kushirikiana na taasisi zinazohusika na uhaulishaji itaendelea kuwasisitiza Viongozi wa Umma na Wananchi kuhusu umuhimu wa uhaulishaji wa mali zao kwa faida yao binafsi na taifa kwa ujumla.

iv. Ugumu wa kupata taarifa au ushahidi kuhusiana na tuhuma au malalamiko ya uvunjaji wa maadili – elimu inaendelea kutolewa kuhusu wajibu wa wananchi katika kuunga mkono juhudi za Serikali katika kuimarisha utawala bora.

v. Kutokukamilika kwa Mfumo wa Kielektroniki wa Usajili wa Taarifa za Mali na Madeni ya Viongozi wa Umma; - Tume ya Maadili kwa

copy

kushirikiana na Wataalamu kutoka Idara ya Serikali Mtandao wanaendelea na kazi ya kuhakikisha mfumo huo unaanza kutumika katika mwaka 2019/2020.

vi. Uhaba wa vyombo vya usafiri kwa ajili ya ufuatiliaji wa kazi za Tume ya Maadili hasa katika eneo la uhakiki wa taarifa za mali na madeni; - Tume ya Maadili imejipangia katika bajeti yake ya kila mwaka wa fedha kununua gari moja. Katika kipindi hiki cha utekelezaji, gari moja imenunuliwa kwa ajili ya Ofisi ya Tume ya Maadili Pemba;

vii. Ugumu wa kuyafikia baadhi ya maeneo ya mali za viongozi wakati wa uhakiki, kutokana na miundombinu ya njia (barabara) na mvua; - Njia mbadala kama vile kutembea kwa miguu. n.k hutumika ili kuhakikisha kuwa mali zilizotamkwa zinahakikiwa.

copy

## 13.0 MIKAKATI YA TUME YA MAADILI KWA MWAKA 2019/2020

Tume ya Maadili imepanga kutekeleza kwa mwaka wa fedha 2019/2020 mikakati ifuatayo:

i. Kukamilisha mfumo wa ndani wa ki-elektroniki utakaotumika katika kusajili na kuhifadhi Taarifa za Mali na Madeni;

ii. Kuhakiki Taarifa za Mali na Madeni ya Viongozi wa Umma;

iii. Kuongeza kasi ya uchunguzi wa malalamiko na tuhuma za ukiukaji wa Sheria ya maadili ya viongozi;

iv. Kuongeza kasi ya utoaji wa elimu kwa Wananchi na Viongozi wa Umma Unguja na Pemba kuhusu umuhimu wa kukuza maadili;

v. Kuwajengea uwezo watumishi wa Tume ya Maadili kwa kuwapatia mafunzo maalum katika maeneo ya Uongozi na Maadili, Usajili, Uhakiki, Uchunguzi, TEHAMA, n.k.;

vi. Kukuza na kuimarisha ushirikiano na uhusiano Kitaifa, Kikanda na Kimataifa; na

vii. Kufanya marekebisho ya Jadweli ya kwanza ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma.

## 14.0 MAPENDEKEZO

Ili kufanikisha utekelezaji wa kazi zake, Tume ya Maadili inapendekeza mambo yafuatayo:

i. Wananchi, viongozi na taasisi zinazohusika waendelee kutoa ushirikiano, taarifa na msaada katika kusimamia na kubainisha ukiukaji wa maadili unaofanywa na baadhi ya viongozi wa umma ili hatua zinazopaswa ziweze kuchukuliwa.

ii. Serikali iendelee kuipatia Tume ya Maadili vitendea kazi ili kuongeza kasi ya ufuatiliaji na utekelezaji wa majukumu yake.

iii. Mamlaka zinazohusika na uhaulishaji wa mali zinazohamishika na zisizohamishika (Bodi ya Uhaulishaji Ardhi, Bodi ya Mapato Zanzibar, Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali, n.k.) zitilie mkazo na kuwashajihisha wananchi kuhusu umuhimu wa kukamilisha taratibu za uhaulishaji, ili taarifa za umiliki wa mali zao uwe sahihi na halali.

copy

## 15.0 HITIMISHO

Suala la usimamizi wa maadili linahusisha viongozi, wananchi na taasisi mbalimbali zinazosimamia utawala bora na zile zinazohusika na masuala mengine ya kijamii. Tume ya Maadili ndio taasisi iliyopewa jukumu la usimamizi wa masuala ya maadili ya viongozi wa umma kwa Zanzibar. Hata hivyo, utekelezaji wa majukumu hayo unategemea kwa kiasi kikubwa ushirikiano na upatikanaji wa taarifa kutoka kwa wananchi na taasisi nyengine.

Tume ya Maadili imekuwa ikipata ushirikiano kutoka kwa viongozi, wananchi, taasisi zinazosimamia utawala bora na zile zinazohusika na masuala mengine ya kijamii. Aidha, Wizara, Idara, Taasisi za Serikali, Viongozi na Watumishi wa Umma wamekuwa ni sehemu muhimu katika kufanikisha utekelezaji wa kazi za Tume ya Maadili. Ushirikiano huo, umechangia na kuisaidia Tume ya Maadili kutekeleza kazi zake kwa ufanisi. Hata hivyo, ushirikiano zaidi unahitajika ili kuleta ufanisi katika utekelezaji wa kazi za Tume ya Maadili na kukuza uwajibikaji kwa viongozi.

Kutokana na taarifa mbalimbali, Tume ya Maadili imeweza kutekeleza kazi zake za kupokea, kusajili na kuhifadhi Tamko la Mali na Madeni kutoka kwa Viongozi wa Umma. Aidha, taarifa hizo zimeiwezesha Tume ya Maadili kufanya uhakiki wa taarifa za Mali na Madeni ya Viongozi wa umma pamoja na kufanya uchunguzi kuhusu malalamiko ya uvunjaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Kwa upande mwengine, kazi ya utoaji elimu kwa umma na viongozi kuhusu umuhimu wa kuimarisha maadili ilitekelezwa Unguja na Pemba katika ngazi mbalimbali zikiwemo Shehia, Skuli, Mabaraza ya Vijana ya Wilaya zote pamoja na Viongozi wa Umma.

copy

Viongozi wa umma ni zao la jamii. Hivyo, jamii ina wajibu mkubwa katika kuwafinyanga, kuwajenga na kuwandaa kimaadili viongozi ambao wanatarajiwa kupewa dhamana za uongozi kwa lengo la kuwatumikia wananchi katika kutimiza mahitaji yao ya kijamii, kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni.

Ripoti hii ya Tatu ya Utekelezaji wa Kazi za Tume ya Maadili imeelezea hali halisi ya utekelezaji wa majukumu yake kwa mwaka 2018/2019. Ni matarajio ya Tume ya Maadili kuwa ripoti hii itasaidia kuongeza uelewa na ufahamu kwa viongozi wa umma, wananchi, taasisi za serikali na zisizo za kiserikali kuhusu majukumu na utekelezaji wa kazi za Tume ya Maadili.

## 16.0 UWASILISHAJI WA RIPOTI


copy

Ripoti hii inawasilishwa kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, **Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein**, kwa mujibu wa kifungu cha 29(1) na (2) cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Nam. 4 ya 2015, leo **tarehe 25 Septemba, 2019**.

**Kwa heshima, naomba kuwasilisha.**

**ASSAA A. RASHID**
**MWENYEKITI**
**TUME YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA**
**ZANZIBAR.**

**Kiambatanisho Nambari 1: Muundo wa Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma**



**Kiambatanisho Nambari 2: ORODHA YA VIONGOZI WA UMMA**

**(Chini ya Kifungu cha 3 cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Nam. 4 ya 2015)**

1. Rais wa Zanzibar
2. Makamu wa Kwanza wa Rais
3. Makamu wa Pili wa Rais
4. Jaji Mkuu
5. Spika wa Baraza la Wawakilishi
6. Mawaziri
7. Mwanasheria Mkuu wa Serikali
8. Manaibu Mawaziri
9. Washauri wa Rais
10. Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi
11. Majaji
12. Kadhi Mkuu
13. Mufti
14. Naibu Spika wa Baraza la Wakilishi
15. Mwenyekiti wa Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar
16. Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi
17. Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali
18. Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango Zanzibar
19. Makatibu Wakuu
20. Mkurugenzi wa Mashtaka
21. Katibu wa Kamisheni ya Utumishi wa Umma
22. Katibu wa Baraza la Wawakilishi
23. Naibu Katibu wa Baraza la Mapinduzi
24. Manaibu Makatibu Wakuu
25. Katibu wa Rais
26. Mkuu wa Mkoa
27. Mkuu wa Wilaya
28. Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar
29. Makamishna wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar
30. Katibu wa Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar
31. Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali
32. Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka
33. Wakurugenzi Wakuu
34. Makamishna (Waajiriwa wa SMZ)
35. Katibu Tawala Mkoa
36. Mhasibu Mkuu wa Serekali
37. Makatibu Watendaji
38. Mtakwimu Mkuu wa Serikali.
39. Msaidizi Mhasibu Mkuu wa Serikali
40. Wakurugenzi
41. Naibu Katibu wa Rais
42. Maafisa Wadhamini wa Mawizara, Idara na Taasisi za Serikali
43. Mameneja na Wakuu wa Mashirika ya Umma Zanzibar
44. Mkemia Mkuu wa Serikali
45. Katibu Tawala Wilaya

copy

46. Mrajis wa Mahkama Kuu
47. Naibu Kadhi Mkuu
48. Naibu Mufti
49. Wakuu wa Idara za Serikali zinazojitegemea
50. Wakuu wa Idara Maalum za SMZ
51. Naibu Wakurungenzi Wakuu
52. Makadhi
53. Mahakimu
54. Manaibu Wakurungezi
55. Makamu Wakuu wa Vyuo Vikuu vya Umma
56. Manaibu Makamu Wakuu wa Vyuo Vikuu vya Umma
57. Wakuu wa Vyuo vya Umma
58. Meya
59. Katibu wa Halmashauri ya Wilaya
60. Katibu wa Mufti
61. Naibu Katibu wa Mufti
62. Katibu wa Tume ya Utumishi Serikalini
63. Katibu wa Tume ya Utumishi ya Baraza la Wawakilishi
64. Katibu wa Tume ya Utumishi ya Mahkama
65. Katibu wa Tume ya Utumishi wa Idara Maalum
66. Wahasibu wa Wizara, Idara na Taasisi za Serikali
67. Wakaguzi wa Ndani wa Hesabu wa Wizara, Idara na Taasisi za Serikali
68. Mwenyekiti wa Bodi ya Zabuni
69. Wasaidizi wa Rais
70. Naibu Wasaidizi wa Rais
71. Makatibu wa Makamu wa Kwanza na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar
72. Manaibu Makatibu wa Makamu wa Kwanza na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar
73. Mganga Mkuu
74. Daktari Dhamana
75. Muuguzi Mkuu Muandamizi
76. Matroni
77. Wajumbe wa Bodi za Vyuo na Taasisi za Umma Zanzibar
78. Maofisa wa Sekretarieti ya Baraza la Mapinduzi
79. Wateule wa Rais na Waziri

copy

| Kiambatanisho Nambari 3: Malalamiko yaliyopokelewa Julai-Juni 2018/2019 | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **SN** | **Aina ya Lalamiko** | **Idadi ya Malalamiko** | **Hatua za Malalamiko** | | |
| | | | **Yaliyopelek-wa Taasisi nyengine** | **Uchunguzi unaendelea** | **Uchunguzi umekamilika** |
| 1 | Rushwa na Ubadhirifu wa mali za umma | 2 | 1 | - | 1 |
| 2 | Matumizi mabaya ya madaraka | 3 | 1 | - | 2 |
| 3 | Shindikizo lisilofaa katika kumfukuza kazi/au kumpandisha cheo mtumishi wa umma | 1 | - | 1 | - |
| 4 | Kutoa taarifa za kikazi kwa watu wasioruhusiwa | 1 | - | 1 | - |
| 5 | Kashfa na matumizi ya lugha ya matusi | 2 | - | 1 | 1 |
| 6 | Kujilimbikizia mali | 1 | - | - | 1 |
| 7 | Udhalilishaji wa kijinsia na Uasharati | 3 | 1 | 2 | - |
| | **Jumla** | **13** | **3** | **5** | **5** |

copy